


# STORIKA THE 50 LEGENDS.

*Be inspired, Document and Share*

**No one cares until someone cares; be that one!**
– Ken Poirot

## WALENGWA

Kwa wazee wote popote walipo wanaodhani na kuona kwamba hawawezi kufanya jambo kwa sababu ya umri wao na kwa vijana wanao shindwa kujihusisha na fursa mbalimbali, amini kwamba yapo mambo mengi mnaweza kufanya. Lakini, kwa mashirika yanayo dhania hawana msaada wowote kwa wazee.

**SHUKURANI**

Tunapenda kutoa maneno ya shukrani kwa Get up that Hill 2022- Ireland community kwa ufadhili wa fedha uliotumika katika kukusanya hadithi zilizopo katika kitabu hichi.

Pia tungependa kutoa shukrani zetu za dhati kwa viongozi wa baraza la wazee mikoa yote Tanzania, viongozi wakijamii na wa asasi za kijamii kwa mchango wao katika kutu tambulisha kwa wazee maleg- endari na kwa jamii pia.

Mwisho kwa vijana walio jitolea na kufanya nasi kazi kwa ukaribu ili kusanya hadithi hizi kwa ubora.

## UJUMBE WA UKARIBISHO.

Tukiwa tunashereka kitabu hiki, tunasherekea shughuli za uandishi, usomaji, tafsiri na uchapishaji, shughuli ambazo zina sadia mtu kuwa na uelewa wa kufanikisha malengo, na kwa hivyo tunasherekea katika njia ya msingi, uhuru ambao umefanikisha mambo mengi. Ungana na sisi tukiwa tunasherekea na wazee waliothubutu kujaribu kufanya bila kujali umri au kasoro.

Ninayo furaha ya kuwa tambulisha Storika, kitabu cha hadithi za malegendari 50 ambacho kitawapatia hamasa na kuwapa moyo wanajamii kufanya kazi kwa bidii bila kujali umri au mapungufu yao. Tumeungana mikono na kupeana ushirikiano katika kukusanya hizi hadithi na sasa tupo hapa kwa ajili ya kusherekea.

Kikubwa cha kujifunza katika usomaji wako wa kitabu hichi ni: tunatafuta mbinu za kuwezesha wazee kupanua biashara zao, kuwakuzia ujuzi wa kutimiza shughuli zao na pia kurahisisha uzajishaji halikadhalika kuwakutanisha na masoko zaidi.

Leo tukiwa tunawatambua na kuwa sherekea hawa 50, wale walio thubutu, ni matamanio yetu kwamba kesho tutawafikia wengi zaidi na kuwasherekea chini ya ushirikiano wetu.
Karibu saveelders.

SARAH EDGAR LAMBA



DATE: 14th April,2023

**Ubunifu kazi za mikono**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Mary B Maira ana umri wa miaka 60, anaishi mkoani Singida, yeye ni mnyaturu kwa kabila. Mary ni kiongozi wa kidini na pia ni kiongozi wa kijamii na ni mwalimu mstaafu wa shule ya Paloti seminary iliopo Singida.

Mary ni legendali kwa sababu amejiajiri, anajituma na anajitambua na pia ni msomi na mbunifu. Anatengeneza shanga, rozari na tasbih kama nyenzo muhimu za kusalia kwa ajili ya wakristo na waislamu. Mara zote huuza kwa waumini wa imani hizo. Mary anasema kua gharama za mwanzo za biashara hiyo ni ndogo sana ukilinganisha na faida anayopata. Mary anapenda kujifunza na anazidi kufurahia kujifunza vitu vipya ukiachana na umri kua mkubwa. Anasema kujifunza kwake ni hatua.

Asante sana Mary, Wewe ni legendari.

*Imeandaliwa na Ismaili Sarumbo (STVolunteer)*



**Mary B Maira**

**Mwandishi wa kitabu na mwasisi wa Kopa Mbuzi**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Abdallah Mohamed Majumba ana umri wa miaka sabini, anaishi Lindi-Tanzania na kabila lake ni Ngindo. Abdallah ni mwandishi wa kitabu kinachoitwa "Ukosefu wa Ulinzi wa Kijamii Tanzania" pia ni mwasisi wa kikundi cha kusaidiana kijamii kinachoitwa 'Kopa Mbuzi, Lipa Mbuzi" lengo likiwa ni kusaidia wazee kujipatia kipato kwa kuuza mbuzi, mtu anaweza kuanzisha mradi wa kufuga mbuzi kwa kukopa mbuzi wa mbegu na hatimaye kuwa rudisha pale watakapokuwa wamezaa mbuzi wengine.

Kilichompelekea Abdallah kuwa msaada kwa wazee wengine ni kutokana na hamasa aliyoipata kutoka kwa babu na bibi wake akiwa na umri mdogo. Swala la kuwasaidia wazee wenzake limempatia utambuzi kwa jamii na kwa shirika la msaada la nchini Australia walioji-tolea katika kuchapisha kitabu cha Abdallah Mohamed.

Asante Abdalah, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Flora Musira (STVolunteer)*



**Abdallah Mohamed Majumba**

**Mfugaji kuku mwenye fahari**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Grace ana umri wa miaka 70, alizaliwa na kukulia Dodoma na bado anaishi huko. Yeye ni mfugaji wa kuku na ndio shughuli inayompatia kipato kwa miaka mingi sasa, anafa-nyia ufugaji huu nyumbani kwake. Yeye ni legendari kwa sababu anajitegemea, ni mbunifu, wa kisasa na pia ame-kuwa bega kwa watu wengine.

Grace ni mtu wa kutoa msaada kwa watu wengine, ameku-wa akiwaelekeza vijana na wazee wengine namna ya kuanza kufuga kuku kwa tija na namna ya kufanya ufugaji endelevu. Ana tumia mbinu za kisasa katika mradi wake, pia ameweza kukuza soko lake kwa kuuza maeneo ya sokoni, ambako anasambaza nyama za kuku pamoja na mayai ya kuku pia. Hili limeweza kumpatia kipato cha kujikimu yeye na familia yake pamoja na kujiwekea akiba kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Asante Grace, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Munira Yusuph (STVolunteer)*



**Grace Mwaja**

## Mkulima wa Mtindo wa Matuta

#TunaKushereKeaweweLeo

Hassan Hausa Mchopa ana umri wa miaka 60, anaishi Lindi-Magome- ni. Hassan ni mkulima mdogo, na amekuwa akitumia kilimo cha aina ya matuta, watu katika jamii yake wamekuwa wakivutiwa na aina ya kilimo anachofanya Hassan na wamekuwa wakimtembelea mara kwa mara kwa lengo la kujifunza mbinu yake, hali khadhalika Hassan amewekeza mashambani Newala-Mtwara. Hassan ni legendari kwa sababu yeye ni mbunifu, ni mtu wa kisasa, ana utayari wa kujifunza jambo jipya na pia ana utayari wa kujaribu jambo jipya.

Hassan alinunua shamba lake akiwa na umri wa ujana na akaanza shughuli ya kilimo baada ya kustaafu kufundisha shule ya msingi. Hivi karibuni alipanda mihogo kwa ajili ya kuuza na matumizi yake binafsi pia. Shughuli za kulima zimemsaidia sana maishani mwake. Jamii inayomzunguka Hassan mtazamo mzuri juu yake kwa sababu yeye ni mchapa kazi, na Anawasihi vijana kuwekeza katika umri huo ili waishi vizuri uzeeni.

Asante Hassan, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Flora Musira (STVolunteer)*



**Hassan Hausa Mchopa**

**Mzalendo wa Kitaifa**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Said Mapesa Mwiyabi ana umri wa miaka 80, anaishi Bariadi-Simiyu na ni mkerewe kwa kabila. Said pamoja na wenzake walikuwa waasisi wa wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu mnamo mwaka 1970. Yeye ni legendari kwa sababu ya uzoefu wake wa uongozi, mpambanaji na Mzalendo.

Katika kipindi chake cha ujana Said alikuwa mwanaharakati wa maendeleo na utaifa, hili limeweza kumpatia nafasi ya kufanya kazi kwa karibu na serikali ya Tanzania, Said alizaliwa Bunda mkoani Musoma, lakini alihamia Bariadi kutokana na migongano ya kijamii. Alijiunga na chama cha TANU mnamo mwaka 1954, kama mwanaharakati wa utaifa, Said alihudhuria kikao cha Azimio la Arusha.

Asante Said, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Time Rashidi (STVolunteer)*



**Said Mapesa**

**Mwezeshaji kwa vijana**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Saimon Simon ana umri wa miaka 70, alizaliwa mkoani Dodoma. Kwa kabila Saimon ni mgogo, anamiliki mradi wa kilimo ambao umeajiri watu wapatao 20 wa vibarua, yeye ni legendari kwa sababu anawawezesha watu, ni mbunifu na mtu wa kutoa msaada.

Saimon amekuwa akiwekeza katika shamba lake kwa kipindi cha miaka sasa, na amekuwa akisafirisha mazao yake shambani yeye mwenyewe huku akisaidiwa na baadhi ya vijana anaowajengea uwezo. Anatueleza kwamba kilimo cha kisasa kina tija na mazao ni mengi na hasara ni chache ukilinganisha na kilimo cha Awali. Kwa sasa anatunza pesa kwa ajili ya kununua mashine kubwa ya kuchakata na kuhifadhi mazao mara baada ya kuvuna, kila la kheri katika hili Saimon.

Asante Saimon, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Munira Yusuph (STVolunteer)*



**Saimon Simon**

**Wakipekee na wakujitoa kwa kazi zake**

#TunaKusherekeaWeweLeo

Hafsa Ismail Kiasile anaishi Ubongo, mkoani Dar es salaam, na ana umri wa miaka 61. Kabila lake ni Mhehe. Anafanya kazi kama Afisa Ustawi wa Jamii, pia ni katibu msaidizi wa kamati ya wazee Tanzania. Hafsa anapenda shughuli za ujasiriamali akiwa amewekeza katika maduka ya Rejareja na nyumba za kupangisha. Yeye ni legendari kwa sababu ya uchapaji kazi wake, uwezo wake wa uongozi na kujitoa kwake katika mambo mbalimbali.

Hafsa ni mfano mzuri wa kuigwa, anasema biashara zake za maduka ya reja reja na nyumba za kupangisha alianza kwa mtaji mdogo wa laki nane na ameweza kukuza mtaji wake kwa muda, ingawa anakumbana na changamoto ya kutokukopeshwa na benki wakiwa na imani kwamba kwa sababu ya umri wake atashindwa kulipa kwa sababu hata kuwa hai muda mrefu. Kwa uzoefu wote huu anastahili kuwa legendari.

Asante Hafsa, wewe ni legendari.

*Imeandaliwa na Jacquiline Raphael (ST Volunteer)*



**Hafsa Ismail Kiasile**

## Nguvu ya kuwa na watoto wanaojali

#TunaKusherekeaWeweLeo
Magreth Samson Higita anaishi Kasulu-Kigoma, yeye ni mlu-fiti kwa kabila. Ana umri wa miaka 70. Magreth ni mjasiria-mali, anamiliki duka eneo la soko na pia ni mkulima mdogo wa mboga za majani katika eneo la nyumbani kwake. Yeye ni legendari kwa sababu anapenda shughuli anazofanya na anaamini kwamba furaha ni kila kitu maishani.

Anasema anapenda sana kuwa na furaha, anajisikia hai zaidi na mwenye furaha pale ambapo akiwa anafanya shughuli zake na kuchangamana na watu sokoni huku wakipiga stori na kucheka. Magreth amebarikiwa kuwa na watoto watano na watoto wake wamekuwa wa msaada sana kwake, na hata hela ya mtaji ya bishara zake alipata kutoka kwa watoto wake, na mpaka hivi sasa bishara zake ni endelevu.

Asante Magreth, wewe ni legendari.

*Imeandaliwa na Christina Kavumvuli (STVolunteer)*



**Magreth Samson Higita**

**Nguvu ya kazi za kujitolea**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Jonas Maneno ana umri wa miaka 74, ni mhudumu wa afya ngazi ya jamii anaishi Mwanza-Tanzania. Jonas amekuwa akijitolea katika kufundisha watu juu ya VVU na maambukizi ya UKIMWI na mambo mengine yanayohusu afya ili kuleta hamasa kwa wanajamii kujijengea mazoea ya kupima afya zao.

Kwa zaidi ya miaka 14 amakuwa akifanya shughuli za kuhamasisha wanajamii wenye umri mbalimbali katika kujitolea kupima VVU na wale wanao ishi namaambukizi waweze kuzingatia matumizi ya dawa, kuzingatia lishe bora na mitindo bora ya maisha. Yeye ni legendari kwa sababu ya uhamasishaji wake na kuwawapa watu moyo na kushirikiana na jamii. Jonas anasema umri sio kigezo cha ukomo, anaendelea kuelimisha watu nyumbani kwake na amejizolea uzoefu wa miaka mingi katika utoaji wa huduma majumbani.

Asante Jonas, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Beatrice Mwijage (STVolunteer)*



**Jonas Maneno**

**Mtafutaji wa fursa**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Elieza Raymond ana umri wa miaka 70, anaishi Arusha, yeye ni mpare kwa kabila. Elieza amewekeza katika mradi wa ufugaji wa kuku. Kwa miaka mingi sasa ameweza kutunza hela na hili limemuwezesha kununua mashine ya kutotolea vifaranga vya kuku.

Lengo lake kununua mashine hiyo ni kwa ajili kuongezea biashara yake thamani, na hivi sasa ameongeza kipato chake kwa kuuza mayai, vifaranga, na kuku kwa ajili ya nyama. Elieza ni legendari kwa sababu ya uwezo wake wa kubaini fursa na kuweza kuzitumia ili kujipatia kipato kwa kupitia fursa hizo. Anasema huwa anajisikia furaha pale vijana wanapokuja kumtembelea nyumbani kwake kwa lengo la kujifunza na kuunga mkono biashara yake.

Asante Elieza, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Flora Masuka (STVolunteer)*



**Elieza Raymond**

**Kuna nguvu katika kujitolea.**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Hamisi Kiza Nyumirwa ana umri wa miaka 70, anaishi Uvinza, mkoani Kigoma. Hamis ni muha kwa kabila. Hamisi ni mwanacha- ma hai wa jamii yake kwa Kupitia nafasi yake ya uongozi katika jamii na dini pia. Pia amekuwa akijitolea kwa miaka mingi sasa na amekuwa kama nguzo katika jamii yake.

Hamisi ni legendari kwa sababu ya ushawishi wake wa kisiasa pamoja na kiuchumi na kimaadili. Pamoja na hayo Hamis amewekeza katika kilimo na shughuli za ujenzi, na hapo zamani aliwahi kuifanya kazi serikali chini ya uongozi wa hayati Mwl. Julius Nyerere kwenye miaka ya 90.

Asante Hamis, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Christina Kavumvuli (STVolunteer)*



**Hamisi Kiza Nyumirwa**

**Kiongozi wa kwaya kanisani**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Paschal Florian Mwarabu ana umri wa miaka 70, ana ishi Morogoro Ifakara, yeye ni mbunga kwa kabila. Paschal ni mwongozaji wa kwaya katika kanisa analosali, na kipaji hicho kilichepua akiwa shule ya msingi, akiwa anajaribu kujitambua ni wapi ataweza kufanania. Paschal ni legend-ari kwa sababu ya ubunifu, kipaji na kujitoa kwake kwa imani yake.

Hapo awali katika maisha yake alikuwa na ndoto za kuwa mwana muziki lakini aliishia kwenda kusomea ualimu na hatimaye kuwa mwalimu wa shule ya serikali. Katika muda wake wa ziada ndipo alijiunga na kwaya ya kanisa na baada ya miaka mingi kupita akawa kiongozi wa kwaya hiyo. Ameweza kutunga ala na nyimbo nyingi kwa ajili ya kwaya yake, Paschal anajisikia mtimilifu kuwa mwanakwaya na kuishi ndoto yake ya kuwa mwana muziki.

Asante Paschal wewe ni legendari.

*Imeandaliwa na Abby Arton (STVolunteer)*



**Paschal Florian Mwarabu**

**Mstaafu mwenye shughuli mbalimbali**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Jumanne Haruni Mabango, kwa jina maarufu “Mzee Kachara“, jina alilopata kutokana na umahiri wake wa kucheza mpira. Kachara ana umri wa miaka 74 na anaishi Kaliua, mkoa wa Tabora, yeye ni muha kwa kabila. Ana ujuzi wa fundi uwashi, kucheza mpira wa miguu, mkulima na pia aliwahi kuwa mpambaniaji uhuru na ni Mzalendo.

Ametumikia taifa lake na serikali yake kwa uaminifu toka mwaka 1961, na ana storI nyingi sana kuhusiana na historia ya taifa letu. Anajivunia serikali na taifa lake la Tanzania kwa kujali wazee, na kwa nafasi yake binafsi amekuwa msaada kwa wengi na mshauri kwa wengi pia.

Asante Jumanne, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Christina Kavumvuli (STVolunteer)*



**Jumanne Haruni Mabango**

**Mwanamke na toroli la biashara**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Marselina Paskali Mroso ni mchaga kwa kabila na anaumri wa miaka 60. Marselina anaishi Sanawari mkoani Arusha. Marselina ana fahamika zaidi kwa jina la mama tembeza na hili lilitokana na shughuli yake ya kujipatia kipato, yeye anauza mihogo na viazi kwa kupitisha mitaa kwa mitaa kwa kutumia toroli. Anatuambia kwamba anafaidi sana kazi yake kutokana na kukutana na watu wapya kila siku.

Shughuli hii imeweza kumpatia kipato cha kuendesha maisha yake na ya familia yake kwa miaka mingi sasa. Yeye ni legendari kwa sababu ya upekee wake na utu wake safi. Shughuli yake ya kusambaza mihogo na viazi mitaa kwa mitaa kwa tolori ni ya kipekee tofauti na kukaa sokoni kusubiri wateja, pia anasema inampatia nafasi ya kufanya mazoezi.

Asante Marselina, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Flora Masuka (STVolunteer)*



**Marselina Paskali Mroso**

**Uwalimu ni wito wa kutumikia binadamu**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Elias Ngwangineza, maarufu kwa jina "Mdau au hamjambo" majina aliyojipatia kutokana na kuchangamana sana na jamii yake Kupitia shughuli mbalimbali. Elias ana umri wa miaka 68 na anaishi Kasulu, mkoani Kigoma, yeye ni muha kwa kabila. Ni kiongozi wa kijamii, msanii na Mwandishi wa vitu mbalimbali.

Elias aliwahi kuwa mwalimu wa lugha za Kiswahili na Kiingereza toka kipindi cha 1976 mpaka kustaafu kwake, ana uzoefu wa miaka mingi wa ufundishaji. Elias Anapendelea zaidi kazi za kujitolea akisema zinampatia baraka na furaha sana kuliko kazi za maslahi. Anasema moja wapo wa kipaji chake cha ufundishaji ni uwezo wake wakuwafanya wanafunzi waone somo zaidi ya nadha- ria na wote walikuwa wanaelewa na kufurahia, amewahi kushinda tunu ya mfanyakazi bora wa mwaka shule ya msingi Akabanga na anajivunia hili mpaka leo hii

Asante Elias, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Christina Kavumvuli (STVolunteer)*



**Elias Ngwangineza**

**Mkulima wa Uyoga.**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Maria Buleji alizaliwa na kukulia Dodoma, yeye ni mgogo kwa kabila. Anaumri wa miaka 75. Shughuli zake ni za kilimo na amewekeza katika kilimo cha uyoga, Ameajiri zaidi ya watu sita wakike kwa wakiume na amekuwa akiwajengea uwezo pia watu 10 juu ya kilimo cha uyoga.

Maria anatumia mbinu kama vile kuuchemsha uyoga, kuanikwa na kisha kufungasha katika mifuko ya plastiki ili kuhakikisha kwamba unadumu muda mrefu bila kuharibika. Anashauri vijana kujikita katika mradi kama huu kwani sio mgumu, unavuna kwa wingi na soko lipo pia ni aina nzuri sana ya chakula chenye thamani mwilini. Kwa kilo moja yeye hupata hadi elfu 12000. Maria ni legendari kwa sababu ya ubunifu wake, uchapaji kazi na uwezo wa kuchangamana na wanajamii

Asante Maria, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Munira Yusuph (STVolunteer)*



**Maria Buleji**

**Fundi wa Ushonaji wa Nguo**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Atanasi Nyimbi anaumri wa miaka 63, ni fundi wa kushona nguo, anaishi Peramiho, mkoani Ruvuma, ni maarufu kwa uchapakazi wake na kuchangamana na jamii yake. Atanasi ni mstaafu, alikuwa mwalimu katika chuo cha ufundi, ana mmiliki duka la nguo, mashine ya kusaga ila pia katika muda wake wa ziaida hufanya kilimo pia.

Kutokana na uchapakazi wake na kujitoa kwake, Atanasi alitunukiwa tunu ya heshima na jamii yake kwa mtaa wao kupewa jina lake "NYIMBI STREET" pia anawashauri vijana kuwa wachapa kazi na wawe na nidhamu ya matumizi ya pesa.

Asante Atanasi, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Janeth Cletas (STVolunteer)*



**Atanasi Nyimbu**

**Kiongozi wa mradi**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Philipo Oswald Katyale alizaliwa na kukulia Peramiho, mkoani Ruvuma. Ana umri wa miaka 68 na anafanya shughuli za kilimo huku akitilia nguvu mazao kama vile mahindi na alizeti. Yeye ni mwasisi wa mradi wa kutoa elimu ya kilimo na afya kwa wazee katika jamii yake na kuwawezesha kujitegemea.

Upekee wa kikundi na mradi wa Philipo unachochea ushirikiano baina ya wazee na kujengeana uwezo katika Nyanja mbalimbali. Anajivunia nafasi yake ya uratibu wa shughuli za mradi kwa sababu kwa sasas wazee wengi wameweza kunufaika na wanajitegemea kiuchumi na kuacha kutegea watoto na wajukuu. Yeye ni lejengari kwa sababu ya uongozi wake, na msaada wake kwa wazee.

Asante Philipo, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Janeth Cletas (STVolunteer)*



**Philipo Oswald Katyale**

**Mfugaji wa kisasa wa nguruwe**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Peter Amos Mkwama maarufu kama Mzee Mkwama, anaishi Iringa Tanzania, ana umri wa miaka 80. Peter amewekeza katika ufugaji wa nguruwe. Anafanya ufugaji huu kwa njia za kisasa kama vile matumizi ya dawa za kuzuia magonjwa mbalimbali, hili limeweza kumsaidia kuwa na kipato cha kuanzia 300000-600000 kulingana na uzito wa nguruwe anayeuzwa.

Peter amekuwa akiwaamasisha vijana wasio na ajira katika jamii yake kujikita katika shughuli za ufugaji wa nguruwe kwa sababu kuna soko na shughuli zake ni nyepesi. Peter alituambia kwamba kuna wakati anauza nyama kwa vipande na kuna kipindi anauza mnyama mzima kulingana na mahitaji ya wateja wake. Yeye ni shujaa kwa sababu ya uwezo wa kubaini fursa katika jamii yake.

Asante Peter, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Munira Yusuph (STVolunteer)*



**Peter Amos Mkwama**

**Fundi Mwashi.**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Adamia Chotipembe Wilagila, Ana miaka 74 na amezaliwa na kuishi Iringa na muhehe kwa kabila. Adamia ni mzoefu wa kazi hii ya mwashi na kwa uhakiki zaidi tumeona baadhi ya kazi zake ni nzuri sana na zinavutia na anatengeneza thamani za nyumbani kama vile, vitanda, viti na meza.
Alipendelea kuwa muwashi baada ya kugundua fursa na rasilimali mbao ambazo zinapatikana kwa wingi Iringa eneo alilopo. Kwa shughuli hizi za Adam saveelders tunamtambua yeye kama legendali. Kwa kupitia kazi zake za mwashi ameweza kutunza na kuhifadhi pesa ambazo ametumia katika uwekezaji ambao unamuongezea kipato. Kwa sasa anamiliki ardhi na nyumba za kupanga za biashara na pia ana mradi wa kufuga kuku. Miaka na miaka amekua akijitoa kuwafunza vijana na wazee katika maswala ya uwekezaji na biashara.

Asante Adamia, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Munira Yusuph (STVolunteer)*



**Adamia Chotipembe Wilagila**

**Fundi viatu**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Phabiano Nyonga anaeishi Babati- Manyara. Phabiano anamiaka 80 na ni Muiraki kwa kabila. Amejiwekeza katika ufundi wa viatu takribani miaka 50 kwasasa. Anafurahia kufanya kazi hiyo sababu kila siku anajifunza na anatengeneza kitu kipya. Kipindi cha nyuma alikua mkandarasi, lakini kutokana na muda aliamua kujiajiri. Ni legendali kwa sababu anafanya shughuli ya utofauti na anajituma.

Anazalisha kipato kupitia biashara yake, na hii inampelekea anaweza kumudu kuhudumia familia yake kama vile kulipia watoto karo ya shule na kuhakikisha familia inapata chakula kila siku. Ni legendari sababu anafanya kazi kwa bidi sana. Alinukuliwa akisema` haijalishi elimu uliyokua nayo, muhimu nikufanya kazi kwa bidii, kua mbunifu na kujituma.

Asante Phabiano, wewe ni Legendari.

*Imeandaliwa na Jessica Ngawe (STVolunteer)*



**Phabiano Nyonga**

**Fundi Baiskeli**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Daniel Bugee, Anamiaka 60. Daniel kwa sasa anaishi Babati-Manyara, kabila lake ni Fyome. Anapoishi baiskeli ni usafiri maarufu na unatumika sana. Na hapo ndipo alipo ona fursa ya yeye kua fundi baiskeli.

Anafanya kazi ya umakini na ya kiwango kikubwa sana na hii imemfanya kua fundi maarufu sana na kumpatia wateja wengi zaidi. Ni legendari kwa sababu ya ubora wakazi yake inayo mpatia wateja zaidi. Anavijana wawili ambao wana-jifunza kutoka kwa Daniel Bugee na kumsaidia kazi. Daniel anasema kua, mara zote wateja wanafika kwake na uhaki-ka wakupata huduma bora, na mara nyingi akisha rekebi-sha baiskeli za wateja ni uhakika wakua haita aribika tena labda tatizo nyingine. Anamiaka 5 toka aanze kazi hii yakurekebisha baiskeli.

Asante Daniel, wewe ni Legendari.

*Imeandaliwa na Ally Nyamhoza (STVolunteer)*



**Daniel Bugee**

**Fundi Umeme wa magari**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Benedict Marandu Appi. Anamiaka 80 na nimzoefu wa kazi za umeme wa magari. Anaishi Babati-Dareda na ni Muiraki kwa kabila. Kwasasa anajihusisha na urekebishaji wa magari mabovu na mashine kubwa kama vile mashine za trekta zinazotumika katika kilimo.

Ni legendari kwa sababu amejituma na kujitahidi katika kutoa huduma ambayo inahitajika sana katika eneo lake na pia ameweza kuajiri na kuwapa mafunzo vijana mbali mbali kuhusiana na umeme wa magari. Alianza kama mkulima ila kwa sasa anamiaka 40 ya uzoefu wa kazi hii ya umeme wa magari. Uzoefu alijifunza kwa baba yake na ndio hivyo nayeye anafunza vijana ujuzi huu.

Asante Benedict, wewe ni Legendari.

*Imeandaliwa na Jessica Ngawe (STVolunteer)*



**Benedict Marandu Appi**

**Matibabu ya asili**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Saidi Mwichande Muhina anafahamika kama Afande, ana-miaka 70 na anaishi Tabora. Ni Mmakua kwa kabila. Amekua bingwa wa dawa za asili katika jamii yake kwa miaka mingi sasa. Anakusanya mizizi na dawa kwenye msitu wa karibu, anatibu mifupa na misuli. Ni legendari kwa sababu ni daktari wa asili na anajivunia anachofanya.

Alipokua na miaka 12, Saidi anakumbuka alimuomba baba yake amfunze namna yakutibu watu kwa kutumia dawa za asili, na hpo ndipo safari yake ilipoanzia kama daktari wa tiba asili. Anaweza kuendesha maisha kwa kupitia huduma hiyo anayofanya katika jamii yake. Miaka wakadha ame-pata wateja kutoka mikoa mbali mbali na mbali zaidi ana-fahamika na mamlaka na kupata kibali cha kutoa huduma.

Asante Saidi, wewe ni Legendari.

*Imeandaliwa na Christina Kavumvuli (STVolunteer)*



**Saidi Mwichande Muhina**

**Mkufunzi wa kilimo**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Jacob Nkandi, anamiaka 70 anaishi Kahama-Shinyanga. Alishawai fanya kazi katika serikali miaka ya 70 katika kitengo cha chakula na Kilimo ila kwa sasa amestaafu. Nkandi ni mkufunzi, na anajitolea kuwafunza wazee wenzake katika kuanzisha bustani za mboga manyumbani. Ni legendari kwa sababu anajitolea na kusaidia jamii

Alitembelewa na saveelders Tanzania mwaka 2022, na kwa pamoja wakaandaa darasa la mafunzo kwa wazee wasio pungua 20 namna ya kuanzisha bustani za mboga majumbani kwa kutumia mifuko. Mafunzo yalikua kwa mifano na saveelders walikuwepo kuhakiki- sha somo linaeleweka na kuwasaidia mahitaji ya awali ya kuanzisha bustani hizo. Nkandi kwa sasa ana bustani ya mfano nyumbani kwake na bado anatoa ushauri na saa kwa wazee wenzake.

Asante Nkandi, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Beatrice Mwijage (STVolunteer)*



**Jacob Nkandi**

**Biashara ya mkaa**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Francis Willium Kifunda anamiaka 69, anaishi Tanga na msambaa kwa kabila. Ameweka muda na pesa katika uuzaji wa mkaa. Anakusanya kutoka kwa wauzaji wadogo na kukusanya katika gala moja ambapo anauza kwa jumla ama rejareja. Ni legendari kwa sababu ya mawazo chanja na kujituma.

Ameanza biashara hii kwa kipindi cha miaka 5, kwake anasema biashara inaenda kwa sababu watu wa eneo lake ni watumiaji wazuri wa mkaa kwa matumizi ya nyumbani kuliko vyanzo vingine vya moto. Kwa siku anaweza kupata mpaka kiasi cha shilling 20000 na hii inatosha kuweza kupata mahitaji yake muhimu. Akinunua wa jumla, hugawa kwa kipimo cha kiasi na kuuza kiasi cha shilingi 2000Tzs. Amejitoa kufanya kazi na anafurahia kufanya kazi.

Asante Francis, wewe ni Legendari.

*Imeandaliwa na Stanley Urassa (STVolunteer)*



**Francis Willium Kifunda**

**Kujitolea kwa jamii yake**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Christopher Hussein Tema anaumri wa miaka 70, na anaishi Bagamoyo, kwa kabila yeye ni Mkwere. Anafanya shughuli za kilimo ila anapenda sana kufanya shughuli za kijitolea kwa jamii inayomzunguka, amekuwa akisaidi makundi yaliyohatarini kama vile wazee, watoto na wanawake, amekuwa akiwasaidia watu wa makundi haya kupitia shughuli za upatanishi, umiliki wa mali pamoja na haki za binadamu.

Mavuno ya shambani kwake yanatosha kulisha familia yake kwa mwaka mzima, ingawa shughuli za kujitolea kwa jamii yake ni matamanio yake kwa miaka mingi sana. Amekuwa akipatanisha watu kwa miaka mingi. Jamii yake imemchagua kuwa muongozaji wa utatuzi wa migogoro, yeye ni legendari kwa sababu ya moyo wake wa kujitolea

Asante Christopher, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Abby Arton (STVolunteer)*



**Christopher Hussein Tema**

**Mtengenezaji wa pombe ya kienyeji.**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Rose Andrew ana umri wa miaka 63. Yeye ni mjasiriamali mdogo na ana miliki duka la nyumbani na bidhaa zinazo-patikana ni kama vile sukari, mchele na chumvi. Pia ana miliki grosari ya kuuza pombe za kienyeji, hii inamsaidia kuendesha maisha yake na ya wajukuu wake.

Katika biashara yake ya pombe za kienyeji ameweza kuajiri vijana 4 ambao wanamsaidi na shughuli za usambazaji wa pombe kwa wateja wake. Pombe hiyo inapatikana kwa jumla na reja reja. Anategema jamii inayomzunguka kama wateja wake, anapata takribani 10,000-15,000 TZS. Kipindi cha likizo ana pata wateja wengi hususani muda wa jioni baada ya watu kutoka shambani watu huwa kujipongeza kwa kazi ya siku.

Asante Rose, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Stanley Urassa (STVolunteer)*



**Rose Andrew Luhui**

**Kujitolea kwa jamii**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Anaitwa Mathew Theobald Msando, alizaliwa na kukulia Moshi Kilimanjaro na ni mchaga kwa kabila. Ana umri wa miaka 70, huwa anajitolea muda wake kufanya shughuli za kijamii kwa kusaidia utunzaji wa watoto wanaotoka katika familia duni na wanaoishi na virusi vya ukimwi kuzingatia dawa. Yeye ni legendari kwa sababu ya shughuli za kuji-tolea.

Alianza kujitolea kuhudumia jamii yake mwaka 2012, na anatuambia kwamba manufaa pekee aliyoyapata ni kama vile kushiriki semina na mafunzo mbali mbali. Katika muda wake wa ziada hufanya kilimo na kujumuika na familia yake. Mara nyingine anapata changamoto pale watu walioathirika wanapogoma kuzin- gatia matumizi ya dawa, anatumia jitahada kubwa kuwashawishi kurejea matumizi ya dawa.

Asante Mathew, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Stanley Urassa (STVolunteer)*



**Mathew Theobald Msando**

**Mjasiriamali**

#TunaKusherekeaWeweleo
Julius Yesaya Nkya ni mtu wa kipekee, hivi sasa ana umri wa miaka 60. Yeye ni mchaga kwa kabila na anaishi mkoani Arusha. Julius ni mjasiriamali, anamiliki duka dogo la mazao ya chakula na bidhaa za viungo.

Ana ishi peke yake, ukiachana na duka lake, Julius ni mfugaji wa kuku na anafanya kazi kwa jitihada ili kuhaki-kisha anapata mahi-taji yake yote. Yeye ni legendari kwa sababu mavuno yake husaidia wazee wenye uhitaji.

Asante Julius, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Flora Masuka (STVolunteer)*



**Julius Yesaya Nkya**

**Mwalimu wa tuition**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Salome S. Bunango almaarufu kwa jina la bibi mwalimu, ana umri wa miaka 75 ni msukuma kwa kabila na anaishi Mwanza. Alistaafu kazi ya uwalimu mwaka 1998 lakini bado ana fundisha katika viwanja vya shule.

Yeye anaamini kwamba umri mkubwa haumfanyi kusahau ujuzi wake alituambia kwamba fagio wa zamani husahau namna ya kufagia. Salome ni legendari kwa sababu hata katika umri wake huu bado amechagua kutoa elimu kwa watoto. Ana ujuzi wa kufundisha lughu za Kiingereza na Kiswahili, anajiskia fahari na furaha kufanya kazi ya ualimu.

Asante Salome, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Beatrice Mwijage (STVolunteer)*



**Salome S. Bunango**

**Mfumaji wa mikeka**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Mwaisha Amani Boli ana umri wa miaka 120, anaishi Lindi-kilwa kisangi. Yeye ni myao kwa kabila. Anatumia muda wake kusuka mikeka kwa ajili ya kupamba nyumba. Kwa jamii yake mikeka hutumika kama sehemu ya mila na tamaduni, inatumika kupamba nyumba na pia inatumika katika shughuli au sherehe za kitamaduni na zinginezo kama vile harusi na mazishi.

Anasema kwamba, alijufunza ujuzi huu zamani kutoka kwa wazazi wake. Amekuwa akifanya shughuli hii kwa muda mrefu na anasuka mikeka mingi sana hata kuweza kugawa mingine bure kwa marafiki na majirani kwa ajili ya kutumika katika shughuli kama vile za mazishi. Anashauri vijana kujikinga na maambukizi ya VVU

Asante Mwaisha, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Sarah lamba (STVolunteer)*



**Mwaisha Amani Boli**

**Mkulima wa mwani.**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Pateki Hamisi Ally ana umri wa miaka 61, anaishi Kilwa katika kisiwa cha Songosongo na Mmatumbi kwa kabila. Amekuwa akifanya kilimo cha mwani kwa zaidi ya miaka 30 ila pia ni mvuvi wa pweza. Ameweza kufanya shughuli hizi mbili kutokana na mazingi- ra ya kazi katika kisiwa alichokulia. Yeye ni legendari kwa sababu ya uthubutu wake.

Anasema anachohitaji katika kuanda mwani ni kamba, fimbo na fito ngumu kwa ajili ya kuchimbia mbegu na kushikilia mwano. Kipindi bahari haijatulia hupumzika kufanya kilimo na badala yake kuchoma na kuuza sambusa nyumbani kwake.

Asante Pateki, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Sarah lamba (STVolunteer)*



**Pateki Hamisi Ally**

**Mfumaji wa vikapu**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Imelda Ibrahim ana umri wa miaka 66, kabila lake ni mhaya, alizaliwa na kukulia kagera katika eneo liitwalo Omukibeta. Imelda ni mjuzi wa ususi wa vikapu ujuzi alionao kwa miaka 44, na alijifunza kutoka kwa mama yake.

Katika makuzi jamii yake inaamini kwamba ususi ni ujuzi ambao msichana anapaswa kuwa nao. Wamama hutumia muda wa mchana baada ya kula kufundisha watoto wao namna ya kufuma. Ameendaleza shughuli hii na anatumia mikono pekee. Anaweza pata mpaka 30000 kulingana na ukubwa wa kikapu. Mara nyingi wateja huwa wanamfuata nyumbani kwake. Imelda ni legendari kwa sababu ya uwezo wa kuona na kutumia fursa.

Asante Imelda, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Christina Kavumvuli (STVolunteer)*



**Imelda Ibrahim**

**Mmiliki wa genge.**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Sabina Moses almaarufu kwa jina la bibi Sungura. Anaumri wa zaidi ya miaka 70, anaishi Tunduru, mkoani Ruvuma, kabila lake ni Mngoni wa asili ya Msumbiji. Yeye anauza mboga za majani na viungo vya mapishi kama vile vitunguu, nyanya katika soko la karibu na nyumbani kwake. Ni mtu anayependa utani na kucheka pia ana uzoefu wa biashara.

Kabla ya kuanza kuuza mboga za majani, alikuwa mtengenezaji wa vyungu, lakini aliachana na hii shughuli pale alipovunjika mkono. Anaona kwamba kuuza mboga za majani ni shughuli rahisi zaidi kwa sababu anapata kipato na mboga zinazobaki anatumia na familia yake. Ana ishi na binti yake ambaye humsaidia katika shughuli za shamba na shughuli za nyumbani. Yeye ni legendari kwa sababu ya kujitoa kwake kwa kazi zake.

Asante Sabina, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Sarah Lamba (STVolunteer)*



**Sabina Moses**

**Mtoa huduma ngazi ya jamii**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Mwasi anaumri wa miaka 70, yeye ni mtu wa vipaji mbalimbali, anaishi Mpakani B, Kijitonyama-Dar es salaam, yeye ni Mzaramu kwa kabila, kwa zaidi ya miaka sita Mwasi amekuwa akifanya kazi kama mtoa huduma za afya ngazi ya jamii kwa kutoa elimu juu ya mambo mbalimbali ya kiafya kama vile VVU, Polio, COVID-19, usafi wa mazingira. Mwasi anamiliki mbinu za kuchangamana na jamii, ni mtu wa kutoa misaada, ni muelewa, mvumilivu na anamapenzi na jamii yake.

Ukiachana na kuelimisha jamii, Mwasi pia ni mshonaji hodari wa nguo. Baada ya saa za kazi hujiunga na rafiki zake katika karakana yao ya kushona nguo ambapo anafanya kazi mpaka usiku. Kwa sasa Mwasi amekuwa akimfundisha binti yake namna ya kuwa mshonaji hodari ili amuachie ujuzi. Shughuli zake mbalimbali zinamuwezesha kupata kipato cha kujikimu. Mwasi ni legendari kwa sababu ya nguvu na jitihada zake za kuelimisha jamii

Asante Mwasi, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Ema Boki (STVolunteer)*



**Muhamed Mwasi**

**Mwenyekiti wa Kitongoji**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Claritha Mrope anaumri wa miaka 65, alizaliwa na kukulia lindi, yeye ni Mwere kwa kabila. Anauzoefu wa zaidi ya miaka 20 ya uzoefu wa uongozi wa kitongoji anachoishi na katika muda wake wa ziada hufanya shughuli za kilimo katika shamba alilorithi kutoka kwa mume wake.

Claritha akiwa kama kiongozi wa kitongoji chake, anau-wezo mkubwa sana wa kutatua kero na migogoro katika jamii yake, na huwa hatozi wananchi wake fedha, tofauti na viongozi wengine ambao hutoza hadi 500o kwa mtu mmoja. Kwa kujitoa kwake wanajamii wake wanampenda sana, yeye ni legendari kwa sababu ya uzoefu wake wa kutatua migogoro katika jamii

Asante Claritha, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Sarah Lamba (STVolunteer)*



**Claritha Mrope**

**Fundi seremala**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Musa Saidi Mamu anaumri wa miaka 80, alizaliwa Mtwara-Nanyumbu, kwa sasa anaishi Tunduru-Nakapanya, mkoa wa Ruvuma na mke wake. Yeye ni fundi useremala hodari na pia ni anachonga vito kwa mbao, alijifunza ujuzi huu kutoka kwa jirani yake ambae ndie aliemfundisha kazi. Musa Alijiunga na chuo cha ufundi kuboresha ujuzi wake wa useremala.

Amekuwa akifanya kazi hii ya useremala kwa zaidi ya miaka 60 na ameendesha maisha yake kupitia shughuli hii. Anajivunia kuwa na huu ujuzi na kwa miaka yote aliyofanya kazi yake pia kwa ubunifu na vitu mbalimbali alivyoweza kutengeneza. Wiki mbili zilizopita alifanikisha kutengeneza viti vya kuvutia sana na kupata wateja 5 ndani ya siku hiyo hiyo. Amefundisha vijana watano huu ujuzi na kwa sasa wanajitegemea na kuendesha maisha yao.

Asante Saidi, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Lea Mponda (STVolunteer)*



**Musa Saidi Mamu**

**Fundi Mhunzi**

#TunaKushereaWeweLeo
Selemani Rashidi Hamis Machopoka maarufu kwa jina la mzee Bomani anaumri wa miaka 70. Alizaliwa Masasi mkoani Mtwara, lakini baadae alihamia Namiungo, wilayani Tunduru, mkoa wa Ruvuma akiishi na wake wake wawili. Amekuwa fundi mhunzi kwa zaidi ya miaka 40 na ni hodari wa kazi yake. Alijifunza kutoka kwa wazazi wake na kitu cha kwanza yeye kutengeneza ilikuwa ni kisu.

Anauhodari wa kurekebisha mashoka na majembe ambayo hutumika katika kilimo kijiji kwake. Alituambia kwamba uhunzi unatumia nguvu sana na kuchosha mwili wake kiasi kwamba anabidi kumeza dawa za kupunguza maumivu mara baada ya kumaliza kazi, zana anazotumia kwa kazi yake ni za mikono. Anatamani wazee wenzake wangeweza kujifunza ujuzi huu ili kujipatia kipato, lakini iatakuwa ngumu kuwezekana kwa sababu kazi inachosha mwili.

Asante Selemani, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Angel Kazula (STVolunteer)*



**Selemani Rashidi Hamis Machopoka**

**Mpishi**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Paul Thomas Kileo anaumri wa miaka 71, anaishi Arusha wilaya ya karatu. Anapenda sana shughuli ya kupika vitafunwa kama vile chips na vinginevyo. Hapo awali alikiwa anapika vitafunwa katika hoteli maarufa ya Kilimanjaro hotel ambayo sasa inajulikana kama Hyatt Regency

Ujuzi huu bado anao hata baada ya kustaafu na umekuwa ukimsaidia kuendesha maisha yake. Anatengeneza vitafunwa na kusambaza katika supermarkets kubwa na hata ndogo katika mkoa anaoishi. Anajivunia kwamba bado anaweza kutumia kipaji na mapenzi yake ya upishi ilikuendesha familia yake na kujipatia mahitaji yake binafsi. Alikuwa ni mpenzi wa kupika toka enzi zake za ujana. Kwa siku anaweza kupika oda mpaka 5-10. Anawashauri vijana kujifunza ujuzi mablimbali katika umri huo na kutafuta fursa mbalimbali badala ya kutegemea ujuzi au shughuli ya aina moja.

Asante Paul, wewe ni Legendari

*Imeandaliwa na Ally Nyamhoza (STVolunteer)*



**Paul Thomas Kileo**

**Mmiliki wa genge**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Savisia Maembe maarufu kwa jina bibi mbogamboga anaumri wa miaka 69 anaishi karatu mkoani Arusha. Yeye anauza mbogamboga na matunda katika kiosk chake lakini pia husambaza matunda. Amefanya shughuli hii tokea 2021 na kabla ya hapo alikuwa anafanya shughuli ya kukaanga na kuuza chips lakini baadae akachana na shughuli hiyo baada ya kushindwa kuhimili moshi wa jikoni kwani amekuwa anatumia kuni.
Aliamua kubadili aina ya shughuli na kuanza kuuza matunda na mbogamboga, anatuambia kwamba kwa siku anaweza kupata wateja hadi 10, na kwamba mbogamboga na matunda haya huyapata kutoka kwa soko la karibu na nyumbani kwake, anayaosha kisha kuyafungasha kwa uweledi na kusambaza kwa wateja wake. Ana-jivunia ubunifu na shughuli yake na kwamba kupitia shughuli hiyo ameweza kuhudumia familia yake na kupata mahitaji yake ya kila siku. Anatamani sana kama angepata kuwezeshwa kuwa na bustani ya mbogamboga nyumbani kwake.

Asante Savisia, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Ally Nyamhoza (STVolunteer)*



**Savisian Maembe**

**Ubunifu kazi za mikono**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Domino Kalolo Tinga anaumri wa miaka 65. Yeye ni hodari wa kufuma bidhaa za ukiri. Amekuwa akifuma vikapu na mikeka kwa kutumia ukiri. Domino anaishi Rukwa mkoani Sumbawanga kwa kabila yeye ni mfipa. Alianza shughuli hii mnamo mwaka 2000 na hivyo anauzoefu wa miaka 23.

Alianza shughuli hii akiwa na umri mdogo na amekuwa akifanya kazi hii kwa oda, lakini pia amekuwa akitafuta wateja wa kuwauzia, kwa siku anaweza kupata oda 5-10. Katika jamii yake watu wamekuwa wakitumia bidhaa za ukiri kama mapambo ya nyumbani na hata kwenye sherehe kama vile harusi. Anaifurahia sana shughuli yake na alitumbia anatumia ubunifu wa hali ya juu ili kuweka uwiano wa rangi za kupendezesha na mali ghafi zingine kwa uweledi na anatumia mikono.
Yeye ni legendari kwa sababu ya kipaji chake na uwezo wa kuendesha familia kwa kipato anachopata.

Asante Domino, wewe ni legendari.

*Imeandaliwa na Reguli Marandu (STVolunteer)*



**Domina Kalolo Tinga**

**Mhunzi wa bidhaa za chuma**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Ezekiel Wayton cheyo anaumri wa miaka 62 anaishi Rukwa-Sumbawanga, yeye ni mundali kwa kabila. Ezekiel ni fundi uhunzi anatengeneza kengele za mifugo na majembe kwa kutumia chuma chakavu. Ezekiel amekuwa akifanya shughuli hii kwa miaka mitatu sasa na anapata fursa ya kuuza bidhaa zake sokoni pia kusambaza majumbani kwa wateja wake.

Alianza shughuli hii baada ya kubaini kwamba umri wake ni mkubwa sana kwa kufanya shughuli ya kilimo. Ana wastani wa wateja 15 na kupata wastani wa elfu 5 kwa siku. Yeye ni legendary kwa sababu amepata njia ya kutunza familia yake katika umri wake na kusomesha watoto wake pia. Angependa kupata msaada wa mtaji kwa sababu soko lake linakuwa.

Asante Ezekiel, wewe ni legendari.

*Imeandaliwa na Reguli Marandu (STVolunteer)*



**Ezekiel Wayton Cheyo**

**Mfumaji wa Mikeka**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Benedict Ngatunga anaumri wa miaka 73. Yeye ni mfumaji kutoka kijiji kilichopo Njombe. Amekuwa akifanya shughuli hii kwa miaka 8 sasa na anauza mikeka anayofuma katika soko la jirani na kijiji chake.

Anapendelea shughuli hii kwa sababu haitumii nguvu sana na inafaa kwa mtu wa umri huu. Inahitaji mikono tu na ujuzi wa kupangilia ukiri kutengeneza mikeka. Anasema kwamba anapata angalua wateja 5 kwa siku. Anapata malighafi kutoka kwenye mazingira yake mwenyewe ambapo anakata nyasi kando ya mto na kuanika ya kauke kisha anayatumia kufumia mikeka hiyo. Yeye ni legendari kwa sababu anatumia firsa katika mazingira yake.

Asante Benedict, wewe ni legendari.

*Imeandaliwa na Daria Magulu (STVolunteer)*



**Benedict Ngatunga**

**Mkulima Mdogo**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Elimina Nikolas Nganju, anaumri wa miaka 78. Anaishi Ludewa, mkoani Njombe. Elimina anamradi mdogo wa kilimo na uzoefu wa miaka 20 katika kilimo.

Alianza shughuli baada ya kukosa msaada kutoka kwa watoto wake baada ya kuvuna mazao yake, anauza moja kwa moja kwa wateja wake ambao mara nyingi humfuata nyumbani kwake hukua akiacha mazao kidogo kwaajili ya matumizi yake binafsi. Mwanzoni alikaribia kukatishwa tamaa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa lakini sasa ameshazoea hali hii. Anauzoefu na bei za soko na pia anapata habari kutoka kwa wakulima wengine pamoja na viongozi wa jamii

Asante Elimina, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Daria Magulu (STVolunteer)*



**Elimina Nikolas Nganju**

**Mjasiriamali**

#TunaKusherekeaWeweLeo.
Kutana na Aneth Kiyando maarufu kwa jina la bibi chiku, anaumri wa miaka 60, na ni Myakyusa kwa kabila. Anaishi Mbeya-Itigi. Anafanywa biashara ya kuuza mchele katika soko la Matola. Anauzoefu wa shughuli hii kwa miaka 12 sasa. Biashara yake ni ya mtaji mdogo, Alichagua kuuza mchele kwa sababu ni bidhaa inayopatikana kwa wingi mkoani Mbeya.

Alikuwa akinunua mchele kwa bei ya jumla na kuuza kwa rejareja na kwa siku anaweza kupata wateja 4-5. Bei za mchele huanzia 1900-2000 kwa kilo moja. Yeye ni legendari kwa sababu ya kuweza kutambua fursa na kuifanyia kazi. Huwa anahakikisha ubora wa mchele anaokwenda kuuza ili wateja wake waridhike.

Asante Aneth, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Catherine Mrema (STVolunteer)*



**Aneth Kiyando**

**Muuzaji wa majiko ya mkaa**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Amos Saidi Mkembela maarufu kwa jina linguine kama iskauke. Ana umri wa miaka 74 na anaishi Mbeya-isanga. Yeye ni Mhehe kwa kabila, anajipatia kipato kwa kuuza majiko ya mkaa katika soko maarufu liitwalo Matola. Amos amekuwa akifanya kazi hii kwa zaidi ya miaka 8. Anasema kwamba wateja wengi ni wenye kipato cha chini. Kwa wiki moja anaweza kuuza majiko 2-3. Majiko anayoyauza yapo imara sana hivyo hategemei wateja wake kurudi kununua jiko linguine hivi karibuni.

Amekuwa akiyanunua haya majiko kutoka katika maduka ya jumla na kuuza kwa rejareja. Anajisikia huru na shughuli yake na hela anayopata anatimiza mahitaji yake huku akiweka na akiba pia. Anasema anafurahi kuwepo sokoni akipiga stori na kucheka na wenzake.

Asante Amos wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Catherine Mrema (STVolunteer)*



**Amos Saidi Mkembela**

**Mjasiriamali mdogo**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Kutana na Nuru Yakobo, anafahamika zaidi kwa jina la bibi mchungaji, anaumri wa maka 70 ana ishi Arusha, yeye ni mmeru kwa kabila. Anafanya kazi kama muuzaji wa viungo vya kupikia na husambaza katika migahawa.

Ana uzoefu wa miaka miwili toka ameanza shughuli hii, alipata hamasa na uhitaji wa mahitaji ya msingi hivyo kuanzisha shughuli ya kujipatia kipato. Ananunua viungo kutoka kwa wauzaji wa jumla sokoni kilombero na kuuza upya kwa rejareja, anajipatia kati ya elfu 10000 na kutunza elfu 5000. Anafaidika kwa kuzunguka mitaani na kukutana na wateja wapya, pia ni fursa ya kufanya mazoezi.

Asante Nuru, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Ally Nyamhoza (STVolunteer)*



**Nuru Yakobo**

**Fundi Seremala**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Yusuph Ayubu anaumri wa miaka 68. Yeye ni mtumbatu kwa kabila na anaishi Zanzibar-mboriborini lakini shughuli zake huzifanyia sebuleni. Yusuph ni fundi seremala na hodari wa kutengeneza vitanda, kwa kutumia kamba. Anauzoefu wa miaka 30-40. Hapo Awali alikuwa askari polisi kabla hajastaafu.

Anatuambia kwamba anamshukuru bibi yake kwani ndie aliyemshau- ri kuwa na kipaji au shughuli nyingine tofauti na ajira yake itakayomletea kipato. Hivi sasa anafanya kazi katika kikundi cha mafundi seremala na wote kwa pamoja wananufaika, kitanda kimoja kinauzwa 45,000 kwa wateja wazawa lakini pia wanauza mahoteli. Ingawa kuna kushuka kwa bei kwa sababu ya misimu ya utalii. Anajivunia kazi yake kwasababu inampatia uwezo wa kujitegemea na kutimiza mahitaji yake, na imemuwezesha kuwekeza katika fursa zingine.

Asante Yusufu wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Abdalla Pandu (STVolunteer)*



**Yusuph Ayubu**

**Kujitolea kwa ajili ya jamii**

#TunaKusherekeaWeweLeo
Wallace Mwakikalo anaishi Kigogo, mkoa wa Dar es salaam. Anaumri wa miaka 70 na ni Mnyakyusa kwa kabila. Yeye ni mstaafu wa hospitali ya taifa Muhimbili alikuwa muuguzi msaid-izi. Hivi sasa anafanya kazi kama katibu wa pension ya wazee wastaafu wa mkoa wa Dar es salaam

Anasaidia wazee wenzake kupata nafasi za huduma ya penshe-ni. Anajivunia kwa fursa alizopata za kujengewa uwezo na kuhudhuria semina mbali mbali za kufundisha uongozi. Kazi yake kubwa ni kuwa kiungani- shi kati ya wazee na serikali. Anakusanya taarifa na kuandaa mikutano mbalimbali. Aliteuli-wa kushika nafasi hii na wazee wenzake waishio kigogo na sasa anawatumikia.

Asante Wallace, wewe ni legendari

*Imeandaliwa na Jacquiline Raphael (ST Volunteer)*



**Wallace Mwakikalo**

# STORIKA
# THE 50 LEGENDS.
*Be inspired, Document and Share*

Malegendari 50.

Tukiachana na changamoto zao mbali mbali, wanazo stori za kusherehekewa leo. Hizi ni stori za malegendari 50. Storika ni kitabu cha uhamasishaji kinacholenga vijana, wazee na taasisi mbali mbali. Kitabu hichi kinabeba jumbe za shughuli na majukumu mbalimbali yanayofanywa na wazee katika jamii yetu ya Tanzania na manufaa yake kwa jamii, uchumi, siasa na tamaduni.

Malegendari 50 ni viongozi wakuhamasisha wengine kufanya kazi kwa bidii na kutokata tamaa. Kwa kuongezea kitabu hiki cha malegendari 50 kinatukumbusha kwamba umri sio kikwazo cha ujuzi na uwezo wa kutekeleza mambi. Kitabu kimewahusisha wazee kutoka maeneo yote ya Tanzania bara na visiwani Zanzibar

Wewe ni legendari tunakusherehekea leo

Designed & Printed by: OGPRO COMPANY LIMITED

SYEAC SMART YOUTH EFFORT FOR ADVANCED COMMUNITY

SAVE ELDERS we are devoted to save them

SaveeldersTanzania
saveelders2016.wordpress.com